**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU – UFUNDI MTWARA.**

Namba ya Simu: 023-2333371
E-mail: mtwarautc@gmail.com
E-mail: mtwara utc@moe.go.tz

S.L.P. 230,
**MTWARA**
13/06/2023

Ndugu

.............................................................
.............................................................
.............................................................
.............................................................

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU ELIMU YA MSINGI NGAZI YA ASTASHAHADA (UALIMU NGAZI YA CHETI) KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024**

## 1.0. UTANGULIZI

Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Elimu ya Msingi Ngazi ya Astashahada (**Ualimu Ngazi ya Cheti**) katika Chuo Cha Ualimu - Ufundi Mtwara kwa mwaka wa masomo **2023/2024.** Mafunzo haya ni ya miaka miwili **(2).**

Mafunzo ya Ualimu Elimu ya Msingi ngazi ya Astashahada (Cheti) ni mhimili muhimu katika mfumo wetu wa Elimu ambapo masomo utakayojifunza yatakujengea uwezo wa juu wa kusimamia mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto.

Mafunzo tajwa yatakuwezesha kutumia mbinu na stadi mbalimbali zitakazowawezesha watoto wa shule za msingi kujifunza kwa ufanisi mkubwa. Mwelekeo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kumwandaa mwalimu mahiri na mwenye ujuzi stahiki katika Elimu ya Msingi. Aidha mafunzo utakayopata yatakupatia sifa na ujuzi wa kufundisha hapa nchini na nje ya nchi kwa kuzingatia fursa za soko la ajira.

## 1:1. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo Mtwara Mjini eneo la Shangani Magharibi (ShanganiWest). Upande wa Mashariki kinapakana na Shule ya Sekondari ya Mtwara Ufundi, Upande wa Kusini kinapakana na Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida (Mtwara K) na Upande wa Kaskazini kinapakana na nyumba za Bodi ya Korosho, nyumba za D.F.I.D na Luwa EverGreen Hotel. Chuo kipo umbali wa mita mia nne (400) kutoka ukingo wa Bahari ya Hindi.

### 1:2. USAFIRI

Kwa wanaosafiri kutokea Dar-Es-Salaam kuja chuoni, baadhi ya mabasi unayoweza kupanda kuja Mtwara ni: **Buti la Zungu, Maning Nice, Tashriff, King Yasin Coach, Machinga Line, Baraka Classic** na mengine. Kwa wanaotokea miji ya Songea, Iringa Mbeya nk, kuja Mtwara wapande magari ya **Seolous/Superfeo**.

NB:

i. Gharama za usafiri kuja chuoni na kurudi nyumbani aidha kwa likizo ndefu na fupi ni juu yako (Mzazi/Mlezi). Hivyo, unashauriwa wakati wa kuja chuoni, kupanda mabasi yanayokuja Mtwara mjini moja kwa moja na siyo mabasi yale yanayoelekea miji ya Masasi, Tunduru, Liwale, Rwangwa, Newala na Nachingwea.

ii. Ukifika kituo cha mabasi Mtwara (**Mkanaledi Bus Terminal**), ili kufika chuoni kwa urahisi, unatakiwa kukodi bodaboda au bajaji kisha mweleze dereva akulete Chuo Cha Ualimu Ufundi Mtwara (maarufu **Mwasandube)**

### 1:3. DIRA YA CHUO

Kuwa ni Chuo Bora kinachotoa Walimu Bora wa shule za Elimu ya Awali na wa Elimu ya Msingi hapa nchini.

### 1:4. MOTTO WA CHUO

Walimu Wapate Stadi

## 2:0. KUFUNGUA CHUO

Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe **17/07/2023**. Endapo utachelewa kuripoti hadi tarehe **31//07/2023 (majuma mawili)** baada ya chuo kufunguliwa, ni bora **USIJE** kwani nafasi yako itakuwa imechukuliwa na mtu mwingine.

## 3:0. MATEGEMEO YETU KWAKO

Kwa hiari yako mwenyewe umechagua kuwa mwalimu. Kwa hiyo unatakiwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za chuo ambazo utaelekezwa ukifika chuoni. Ukienda kinyume na taratibu hizo, uongozi wa chuo hautasita kukuchukulia hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kukuachisha mafunzo.

## 4:0. TARATIBU ZA KITAALUMA CHUONI.

Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na nje ya darasa bila kukosa. Pia unatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote itakayotolewa na wakufunzi na unatakiwa kufaulu kwa kiwango kitakachoelekezwa. Kushindwa kutimiza hayo kunaweza kukusababishia kushauriwa vinginevyo.

## 5:0. MAAGIZO MUHIMU

### 5:1. AFYA YAKO

Unatakiwa kupima afya yako katika **Hospitali ya Wilaya au Mkoa** kabla ya kuja chuoni. Hakikisha fomu ya uchunguzi wa afya yako imejazwa kikamilifu na kuja nayo chuoni na kuikabidhi kabla ya kusajiliwa. Aidha, **unatakiwa kuja na kadi ya Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) au uje na fedha shilingi 50,400/= (Hamsini elfu na**

**mia nne tu) ili uongozi wa chuo ukusaidie kupata kadi hiyo ya Bima ya Afya ya Taifa (NHIF). Hili ni agizo na siyo suala la hiari.** Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya Chuo ya NBC.

**5:2. VIFAA VYA DARASANI**

i. Daftari kubwa zisizopungua kumi na tano (15)- Quire 2 kwa kila moja.
ii. Kalamu za wino na za risasi za kutosha.
iii. Mkebe wa vifaa vya Jometri (Mathematical Set).
iv. Rula ndefu
v. **Rimu moja** (1) ya karatasi za **'Photocopy' A4** zenye karatasi si chini ya **mia tano (500)** kwa ajili ya majaribio.

**5:3. VIFAA VYA MABWENI.**

i. Shuka mbili (2) za rangi ya maji ya bahari (Light Blue)
ii. Chandarua, Taulo na Mto.
iii. Utashirikiana na wanachumba wenzio kupata pazia kwa ajili ya dirisha la chumba chenu. Utaratibu wa ushirikiano huo utaelekezwa ukisharipoti na kusajiliwa hapa chuoni.

**5:4. VIFAA VINGINE VYA LAZIMA.**

i. Ndoo 2 kwa ajili ya matumizi yako (yaani 1 ya maji ya kunywa na 1 ya kuogea).
ii. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko (visiwe vya udongo) kwa ajili ya chakula
iii. Tochi

**5:5. SARE ZA CHUO**

**WANAWAKE**

i. **Sketi mbili za rangi ya buluu nyeusi (dark blue)** zenye urefu wa kutosha na rinda moja la **V** mbele **(Rejea kiambatisho (a) ukurasa namba 7 wa fomu hii hapo chini)**
ii. Mashati mawili ya rangi ya maji bahari (light blue) ya mikono mirefu **yawe ya dukani na si vinginevyo** na tai fupi nyeusi.
iii. **Viatu vya ngozi rangi nyeusi** jozi mbili vyenye visigino vifupi na vipana vinavyofunika miguu na soksi ndefu nyeupe jozi mbili.
iv. Kwa wanachuo wa kike wanaovaa hijab, waje na nusu kanzu mbili ndefu zisizobana maungo na juba mbili ndefu na vingine kama ilivyoelekezwa hapo juu isipokuwa **tai.**
v. Unatakiwa kuja na **Tsh. 15,000/=** kwa ajili ya kupata T-shirt rangi ya Buluu Bahari (Light blue) na maelezo yake yametolewa huko mbele
vi. Unatakiwa uwe na Sweta rangi ya buluu nyeusi "**dark blue**'.

**WANAUME**

i. **Suruali mbili za rangi ya buluu nyeusi (Dark blue)** zenye rinda mbili mbele na chini ziwe na upana wa sm 7 kwa 14 (**Rejea kiambatisho (b) ukurasa namba 7 wa fomu hii hapo chini**). Ukishona suruali ya kubana kinyume na upana huu utanyang'anywa.

ii. Mashati mawili rangi ya maji ya bahari **(light blue)** ya mikono mirefu **yawe ya dukani na si vinginevyo** na **tai** nyeusi ndefu.

iii. **Viatu vya ngozi rangi nyeusi** vinavyofunika miguu jozi mbili na mkanda wa ngozi mweusi au kahawia (brown) na soksi za rangi nyeupe jozi mbili.

iv. Fulana (Tshirt) rangi ya maji bahari (light blue) na maelezo yake yametolewa hapo chini.

v. Unatakiwa uwe na Sweta rangi ya buluu nyeusi "**dark blue**'.

**Zingatia:**

1) **Kila mwanachuo anatakiwa kulipia sh 15,000/= katika akaunti Namba ya michango iliyopo NBC kwa ajili ya T-shirt ya chuo.**
2) **Chuo cha Ualimu Ufundi Mtwara kipo karibu sana na Chuo Cha Ualimu Mtwara K. Kwa ukaribu huu, baadhi ya wanachuo wanaojiunga na chuo chetu huchanganya sare kwa kununua sare ya chuo cha jirani badala ya chuo hiki. Hivyo, zingatia maelekezo ya aina ya sare hapo juu na ukishindwa ni vema uje utafute sare huku Mtwara.**

**5:6 NGUO ZA MICHEZO.**

Uje na T-shirt (1) mpya nyeupe; bukta (1) nyeusi; raba nyeupe na soksi nyeusi jozi (1) kwa ajili ya michezo. Pia uje na '**Track suit'** Buluu Nyeusi **(Dark Blue)**.

**5:7. VYETI MUHIMU.**

Unatakiwa kufika na nakala ya cheti cha kidato cha nne au/na cha sita kwa yule aliyefikia kiwango hicho cha elimu na **siyo result slip** isipokuwa kwa aliyemaliza **mwaka 2022 tu ndiye anatakiwa kuja na result slip**. Pia lete ya cheti cha kuzaliwa, **Usipoleta vyeti hivi hautapokelewa chuoni.**

**5:8. ADA YA MAFUNZO NA MICHANGO MUHIMU YA CHUO**

1. Ada ya Chuo Tsh. 450,000/= kwa mwaka
2. Mchango wa Serikali ya Wanachuo Tsh. 5,000/= kwa mwaka
3. Mchango wa Huduma ya kwanza Tsh. 10,000/= kwa mwaka
4. Mchango wa Usafi na Mazingira Tsh. 20,000/= kwa mwaka
5. Mchango wa Kukodi Godoro Tsh. 10,000/= kwa mwaka
6. Mchango wa Usajili na Kitambulisho Tsh. 20,000/= kwa mwaka
7. Mchango wa Michezo Tsh. 30,000/= kwa mwaka

8. Mchango wa Ulinzi Tsh. 30,000/= kwa mwaka
9. Mchango wa Ukarabati Tsh. 25,000/= kwa mwaka
10. Mchango wa Bima ya Afya (NHIF) 50,400/= kwa mwaka

**JUMLA YA MICHANGO YOTE NI 215,400/=**

**NB: Malipo yote yafanyike BENKI kwa mchanganuo ufuatao**:

1. ADA YA CHUO Tsh **450,000/=** kwa mwaka utailipa kwa **"Control Number"** mara baada ya kufika chuoni au wasiliana na Mhasibu wa chuo kwa namba **0786882067 au 0715882069 ili kupata "Control Number"**.

2. Jumla ya Tsh. **215,400/=** ilipwe kwenye akaunti ya Chuo ya Benki ya kwenye Akaunti namba: ***034103002073. Jina la Akaunti ni MFUKO WA CHUO CHA UALIMU (U) MTWARA***. **Hakikisha malipo yanafanywa kwa kuandika jina la Mwanachuo** husika kwenye risiti ya benki na siyo vinginevyo (siyo jina la mtumaji kama aliyetuma siyo mwanachuo mwenyewe). Fedha hii ikishalipwa hairudishwi.

**5:9. USAJILI**

Ufikapo Chuoni, muone **MSAJILI** wa wanachuo ukiwa na vitu vifuatavyo: barua hii ya kujiunga na chuo, risiti za Benki ulizofanyia malipo (**Bank pay in slips**) zinazoonesha malipo ya michango yote na endapo utalipia kiasi bila makubaliaano au hautolipa kabisa hautapokelewa. Kuwa makini na fedha na mali zako ufikapo chuoni na wakati wote utakapokuwa chuoni.

**Kwa mawasiliano piga 0788033616 // 0766944232 // 0717233679**

**Tunakutakia safari njema ya kuja chuoni na KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU UFUNDI MTWARA**

**SHAIBU.M. AFELI**
**MKUU WA CHUO**
0784 415312

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**PART A:**

TO: The Medical Officer,

..................................................
..................................................
..................................................

From: The Principal,
Mtwara Technical T.C.
P. O. Box 230,
**MTWARA.**
Date: ..........................

**Mr/Miss/Mrs**..........................................................................
(Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course. The examination should include the following categories (I – IV) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect.

Pregnancy (Category IV) will also render a girl ineligible for the course.

(i) (a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy

(ii) Neuroses (iii) Other serious diseases (iv) Pregnancy

..........................................................................................................................
..........................................................................................................................

**PART B:**
**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)
I have examined the above named and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for a full-time teacher training course.

Eye-sight ..............................................................
Hearing ................................................................
Limbs ..................................................................
Venereal diseases....................................................
Leprosy ................................................................
Epilepsy................................................................
Neuroses ..............................................................
Other serious diseases ...............................................
Pregnancy ..............................................................


Date ......................................  Signature ..............................................

Station ...................................  Designation ............................................


MKUU WA CHUO MUFUNDI S.L.P 230

## KIAMBATISHO NAMBA MOJA (1)

a) **Sketi**



b) **Suruali**



MKUU WA CHU... ...MU UFUNDI
S.L.P 230
M...